*Mulika, Na. 44 (1), 95-113*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Uchunguzi wa Ufundishaji wa Stadi za Kusoma na Kuandika katika Utekelezaji wa Mtaala Egemeo Uwezo nchini Rwanda

*Concessa Mukashema*[1] *na Laurien Tuyishimire*[2]

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na44t1.6

## Ikisiri

Ufundishaji mwafaka wa stadi za kusoma na kuandika ni msingi wa kufanikisha Mtaala Egemeo Uwezo (kuanzia sasa MEU) katika somo la Kiswahili. Stadi hizi zinawawezesha wanafunzi kutumia Kiswahili katika mawasiliano rasmi na yasiyo rasmi, na kufanikisha shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi zinazohitaji matumizi ya Kiswahili. Makala haya yanalenga kuchunguza namna ufundishaji wa stadi za kusoma na kuandika unavyofanyika ili kutekeleza MEU. Makala pia yamelenga kueleza changamoto za ufundishaji wa stadi za kusoma na kuandika katika shule za sekondari za wilaya ya Nyamagabe, Rwanda. Mbinu za usaili, ushuhudiaji na uchambuzi wa matini zimetumika ili kukusanya data[3] za kitaamuli, ambazo zimechambuliwa kimaelezo kwa kuongozwa na Nadharia ya Utamadunijamii ya Vygotsky. Matokeo ya utafiti yameonesha kuwa walimu wanatumia mbinu za ufundishaji ambazo haziwashirikishi wanafunzi kukuza stadi za kusoma na kuandika kwa ufanisi. Baadhi ya changamoto zilizobainika ni ukosefu wa vifaa vya kufundishia na wanafunzi kutokuwa na utamaduni wa kusoma. Hivyo, makala yamependekeza njia za kufanikisha ufundishaji wa stadi za kusoma na kuandika. Mapendekezo hayo ni kutumia kazi za andaa – shiriki - tafakari, na usomaji na uandishi changizi.

## 1.0 Utangulizi

Mabadiliko ya haraka katika soko la ajira yanayotokana na maendeleo ya teknolojia na utandawazi duniani, yameleta changamoto katika sekta ya elimu (Mulenga na Kabombwe, 2019). Ili kukabiliana na changamoto hizo, wadau wa sekta ya elimu walifanya jitihada za kutafuta mbinu za kutumika ili kuwaandaa wahitimu wa elimu wenye uwezo wa kushindana katika soko la ajira. Kwa lengo la kufanikisha suala hili, nchi mbalimbali duniani zilianza kutekeleza MEU.

Kwa mujibu wa REB (2015), MEU ni mtaala wenye lengo la kumwaandaa mwanafunzi kuwa na uwezo wa kutatua matatizo atakayokutana nayo katika maisha yake ya kila siku. Aidha, Nzima (2016) anasisitiza kwamba MEU unajenga

[1] Mhadhiri Msaidizi, Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Rwanda, Rwanda. Baruapepe: concessamukashema@gmail.com
[2] Mhadhiri Msaidizi, Chuo Kikuu cha Rwanda, Rwanda. Baruapepe: tulaurien@gmail.com. ORCID: https://orcid.org/0009-0001-0530-4607
[3] Data iliyotumika ilitokana na tasnifu ya Shahada ya Umahiri (2022).

uwezo wa mwanafunzi kuwa mbunifu na kutumia stadi anazojifunza darasani ili kukabiliana na matatizo ya kimaisha. Maelezo haya yanamaanisha kwamba MEU unalenga kumwezesha mwanafunzi kutumia maarifa ya darasani kwa ufanisi katika hali halisi za maisha.

Katika muktadha wa mtaala, uwezo unamaanisha hali ya kutumia muunganiko mwafaka wa maarifa, stadi, maadili na mwenendo mwema ili kufanya kazi kwa ufanisi. Kwa maneno mengine, ni uwezo wa kutumia maarifa ya darasani katika miktadha mbalimbali. Kwa mfano, uwezo wa mwanafunzi kuwasiliana na wengine kwa ufasaha katika hali mbalimbali za maisha kuliko kuelewa sheria za sarufi na kutaja orodha ya msamiati (REB[4], 2015).

Mnano mwaka wa 2015, Rwanda ilianza kutekeleza MEU ili kuwaandaa wahitimu wa viwango mbalimbali vya elimu kuwa na uwezo wa kutumia maarifa ya darasani katika maisha halisi. Mojawapo ya uwezo uliotiliwa mkazo ni wa kimsingi.

Kwa mujibu wa REB (2015), uwezo wa kimsingi unaoanishwa katika nyaraka za sera ya taifa na unatoa mwongozo wa masomo yanayopaswa kupewa kipaumbele na aina ya mwanafunzi anayetarajiwa mwishoni mwa kila ngazi ya masomo. Uwezo huu ni kusoma na kuandika. REB (2015) inaeleza kwamba stadi za kusoma na kuandika zinamwezesha mwanafunzi kusoma maandishi tofauti haraka na kwa usahihi, kueleza mawazo na ujumbe kupitia maandishi yanayoeleweka, kuwasilisha mawazo kwa ufanisi kupitia mazungumzo kwa kutumia fonetiki sahihi, na kusikiliza kwa makini ili kuelewa na kutafuta ufafanuzi zaidi inapohitajika. Maelezo haya yanamaanisha kwamba uwezo huu wa kimsingi ni muhimu katika kufanikisha MEU hususani katika masomo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Kiswahili.

Kiswahili ni lugha ya pili inayofundishwa katika shule za sekondari nchini Rwanda na kutahiniwa katika mitihani ya kitaifa katika kidato cha sita. Kwa mujibu wa REB (2022), lengo kuu la kufundisha Kiswahili ni kukidhi mahitaji ya nafasi yake katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kiswahili kimepewa nafasi kubwa katika ukanda huu kutokana na mchango wake katika kujenga ushirikiano wa kibiashara, kijamii na kitamaduni kuliko lugha yoyote.

Wanafunzi wanaojifunza Kiswahili nchini Rwanda wataweza kuitumia katika mawasiliano rasmi na yasiyo rasmi. Hii itawawezesha kufanikisha shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi zinazohitaji matumizi ya Kiswahili. Baadhi yake ni tafsiri na ukalimani, uandishi na utangazaji habari, biashara na nyanja

[4] REB ni kifupisho cha Bodi ya Elimu ya Msingi ya Rwanda

nyinginezo. Hivyo basi, ufundishaji mwafaka wa stadi za kusoma na kuandika kama uwezo wa kimsingi, utafanikisha MEU hususani katika Kiswahili.

## 2.0 Stadi za Kuandika na Kusoma

Uandishi ni mchakato wa kuzalisha mawazo kwa njia ya maandishi. Kwa mujibu wa Brown (2001), uandishi unahitaji kufikiri kwa kina, maandalizi makini na marekebisho ya mara kwa mara ili kuboresha maudhui. Urquhart na McIver (2005) wanaongeza kwamba kuandika ni mchakato unaojirudia ambapo wanafunzi wanasaidiwa na walimu kuzalisha mawazo yenye maudhui maalumu kimaandishi. Katika mchakato huu, wanafunzi wanapitia katika hatua tofauti ikiwa ni pamoja na kupanga mawazo, kufanya marekebisho, na kuhakikisha maandishi yana maana kwa wasomaji (Kitchakarn, 2014).

Harmer (2004) anaeleza umuhimu wa kujifunza kuandika kwa wanafunzi. Miongoni mwa faida anazozitaja ni: mosi, kuandika kunawapa muda wa kufikiria kwa kina wanapofanya mazungumzo yanayohitaji majibu ya moja kwa moja. Pili, huwawezesha kutumia vifaa vya marejeleo kama vile kamusi na vitabu vya sarufi ili kuimarisha lugha kwa ufasaha. Hatimaye, uandishi huwahimiza wanafunzi kuzingatia matumizi sahihi ya lugha, hivyo, wanakuza uwezo wao wa kuandika. Maelezo haya yanamaanisha kwamba ujifunzaji wa stadi za kuandika unawasaidia wanafunzi kuwasiliana kwa ufanisi kimaandishi katika lugha lengwa.

Kwa upande mwingine, kusoma ni mchakato wa kuelewa ujumbe wa maandishi na dhamira ya mwandishi. Kwa mujibu wa Alderson (2000), ili msomaji aweze kuelewa ujumbe uliopo katika maandishi, anapaswa kufikiri zaidi kila sentensi iliyoandikwa. Miricho (2008) anaeleza kuwa stadi ya kusoma inahusisha uwezo wa mwanafunzi kusoma maandishi kwa mtiririko mzuri bila kusitasita na kutumia sauti inayosikika na matamshi bora ya lugha husika.

Msomaji anasoma akiwa na madhumuni mbalimbali. William na Fredrika (2012) wanaeleza kwamba malengo ya kusoma ni pamoja na kutafuta taarifa, kujifunza kutoka kwenye maandishi, kuunganisha taarifa, kuandika, kuhakiki matini na kusoma kwa ufahamu wa jumla.

Aidha, usomaji unaweza kufanyika kwa namna tatu: mosi, kusoma kwa kimya, ambapo msomaji husoma bila kutoa sauti. Usomaji huu unaweza kujumuisha sauti ndogondogo au hotuba kimya za ndani zinazofanywa na msomaji anaposoma andiko. Pili, kusoma kwa sauti, ambapo msomaji husoma kwa kutoa sauti kubwa ili kufurahia na kukuza stadi ya kusoma. Kadiri mwanafunzi anavyosoma kwa sauti, hufurahia matini na kuboresha stadi za kusoma na kuifahamu lugha zaidi. Aina ya mwisho ya usomaji ni kusoma kwa kina ambako kunahusisha kuelewa ujumbe wa matini inayosomwa na kuuhusisha na miktadha mbalimbali (Bojovic, 2008; Dalaney, 2008).

Uandishi na usomaji ni stadi zinazokamilishana. Hii ni kwa kuwa kusoma kunamsaidia mwanafunzi kupata kuelewa ujumbe wa maandishi huku uandishi ukimpa mwanafunzi fursa ya kutumia maarifa anayojifunza katika miktadha mbalimbali ya maisha. Zaiter (2019) anaeleza kwamba mwanafunzi ambaye hana uwezo wa kusoma kwa ufasaha, anapata pia changamoto katika kuandika. Stadi hizi zinapofundishwa kwa ufanisi, zinawasaidia wanafunzi kupata matokeo mazuri katika masomo na kuwaandaa katika maisha ya kila siku. Hii ni kwa sababu stadi hizi zinawawezesha wanafunzi kuwasiliana kwa ufanisi. Hivyo basi, ni muhimu kutafiti namna stadi hizi zinavyofundishwa hasa kwa wanafunzi wa lugha ya Kiswahili nchini Rwanda ili kuwaandaa kuwa na umilisi wa mawasiliano kama lengo la mtaala tumizi.

## 3.0 Changamoto za Kufundisha Stadi za Kusoma na Kuandika

Stadi za kusoma na kuandika zinakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zinaathiri uwezo wa wanafunzi kwa kuwafanya washindwe kumudu stadi hizi muhimu. Changamoto ya kwanza ni ukosefu wa vifaa vinavyohitajika katika ufundishaji. Ruterana (2012) anaeleza kwamba kuna uhaba wa vifaa vya kufundishia kusoma na kuandika. Aidha, hakuna maktaba za kutosha ambazo zinaweza kutumiwa katika mchakato huu. Hali hii inaathiri vibaya uwezo wa wanafunzi kujifunza lugha kwa ufanisi.

Changamoto ya pili ni ukosefu wa motisha miongoni mwa wanafunzi. Motisha hufasiliwa kuwa ni mchakato wa usimamizi uliopangwa, ambao unachochea watu kufanya kazi kwa uwezo wao (Tremblay, Blanchard, Taylor, Pelletier na Villeneuve, 2009). Hii ina maana kwamba motisha inahusiana na nia, utashi na hiari ya mtu kushiriki katika shughuli fulani, hali ambayo inahusiana na stadi za kusoma na kuandika. Gardener (2000) anadokeza kuwa ukosefu wa motisha miongoni mwa wanafunzi unakwamisha ukuzaji wa stadi za kusoma na kuandika. Hii inaashiria kwamba walimu wanapaswa kutumia mbinu zinazowahamasisha wanafunzi kushiriki kikamilifu katika mchakato wa kusoma na kuandika wanapofundisha masomo yao.

Changamoto ya tatu ni uwezo wa walimu kufundisha stadi hizi. Kwa mujibu wa Jonson (2001), mwalimu anapaswa kuwa na sifa stahiki za kitaaluma zinazohitajika kufundisha somo lake kwa ufanisi, ikiwa ni pamoja na stadi za kusoma na kuandika. Pia, Fema (2003) anabainisha kuwa ukosefu wa walimu wenye uwezo unasababisha makosa ya kimaandishi na kimaongezi kwa wanafunzi. Hii inaonesha athari ya changamoto hii katika ujifunzaji wa lugha. Hivyo, ni muhimu kuwa na walimu wenye uwezo wa kufundisha kikamilifu ili kuwasaidia wanafunzi kukuza stadi za kusoma na kuandika.

Kwa muhtasari, tafiti hizi zimebainisha changamoto zinazokwamisha ufundishaji wa stadi za kusoma na kuandika. Changamoto hizi ni pamoja na ukosefu wa vifaa

vya kufundishia, uhaba wa walimu wenye sifa stahiki na ukosefu wa motisha miongoni mwa wanafunzi. Hata hivyo, tafiti hizi hazijahusisha changamoto hizi na lugha yoyote, kiwango cha elimu au muktadha wa nchi mahususi. Kwa kuzingatia pengo hilo, makala yetu yanalenga kueleza changamoto za ufundishaji wa stadi za kusoma na kuandika katika lugha ya Kiswahili katika shule teule za sekondari wilayani Nyamagabe, nchini Rwanda.

**4.0 Methodolojia na Nadharia ya Utafiti**

Data zilizoibua makala yetu zililenga kufanikisha malengo mawili mahususi: kuchunguza namna ufundishaji wa stadi za kusoma na kuandika unavyofanyika ili kufanikisha MEU na kueleza changamoto za ufundishaji wa stadi za kusoma na kuandika katika shule teule za sekondari za wilaya ya Nyamagabe, Rwanda. Ili kufanikisha malengo haya, data za kitaamuli zilikusanywa kwa walimu wa Kiswahili na manaibu wakuu wa shule wanaohusika na masuala ya taaluma. Shule hizi zimepatikana kwa kutumia usampulishaji lengwa. Kwa mujibu wa Creswell (2012), hii ni aina ya usampulishaji ambapo uchaguzi wa watoataarifa wa utafiti unadhamiria kuwapata watu wanaofikiriwa kuwa watawezesha kupatikana kwa taarifa faafu zinazohusiana na suala linalofanyiwa utafiti.

Hivyo, shule hizo tatu zimeteuliwa kutokana na sababu zifuatazo: mosi, shule hizi ziko karibu na kambi ya wakimbizi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ambapo wengi hutumia Kingwana, mojawapo ya lahaja za Kiswahili (Kipacha, 2003). Hii huwafanya wanafunzi kuwa karibu na wazungumzaji wa Kiswahili. Ni muhimu kufundisha stadi za kusoma na kuandika kwa ufanisi ili kuimarisha uwezo wa mawasiliano katika lugha hii. Pili, shule kuwa na mchepuo wa lugha ambapo Kiswahili ni mojawapo ya masomo ya kutahiniwa katika mtihani wa taifa. Walimu wanapaswa kuwasaidia wanafunzi kuwa na umilisi wa stadi hizi kwa kuwa utawasadia kufaulu mtihani na kuimarisha mawasiliano. Aidha, kigezo cha utofauti katika maeneo kimezingatiwa. Nzima (2016) anabainisha kwamba katika utafiti wa kitaamuli, utofauti wa kimaeneo unasaidia kutoa taswira kuhusu hali halisi katika maeneo tofauti. Kigezo hiki kimesaidia kuchunguza namna muktadha wa kijiografia unavyoathiri ufundishaji wa stadi za kusoma na kuandika katika Kiswahili.

Kwa kuzingatia vigezo hivi, utafiti ulishughulika na shule tatu za sekondari ambazo ni shule ya Mtakatifu Nicolas Cyanika, Mtakatifu Kizito Gikongoro pamoja na shule ya sekondari ya Gasaka. Watoataarifa walikuwa sita yaani, walimu watatu wa Kiswahili na manaibu wakuu wa shule wanaohusika na masomo kutoka shule hizo. Idadi ya walimu wa Kiswahili na viongozi wa shule inalingana na idadi ya shule kutokana na kwamba nchini Rwanda, mara nyingi kila shule huwa na mwalimu mmoja wa Kiswahili na naibu mkuu wa shule anayehusika na masomo mmoja.

Data za kitaamuli zilikusanywa kwa kutumia mbinu tatu ambazo ni uchambuzi wa matini, usaili na ushuhudiaji darasani. Uchambuzi wa matini ulilenga kuchunguza namna ufundishaji wa stadi za kusoma na kuandika unavyofanyika katika Kiswahili. Hivyo, maandalizi ya masomo na nyenzo zinazotumiwa na walimu wa Kiswahili zimechambuliwa ili kuelewa namna stadi hizi zinavyofundishwa.

Vilevile, mbinu ya usaili ilitumika katika ukusanyaji wa data. Mbinu hii ilihusisha mahojiano na walimu wa Kiswahili pamoja manaibu wakuu wa shule wanaohusika na masomo. Usaili na walimu wa Kiswahili umebainisha mbinu wanazotumia kufundisha stadi za kusoma na kuandika, na changamoto zinazowakumba. Kwa upande wa manaibu wakuu wa shule wanaohusika na masomo, usaili umesaidia kupata maelezo ya kiutawala yanayohusu mchakato wa ufundishaji wa stadi hizi. Usaili wa viongozi hawa ulifanyika kwa Kiingereza kwa kuwa wengi wao hawaelewi Kiswahili na wamejifunza masomo tofauti na lugha.

Kadhalika, ushuhudiaji darasani ulifanyika ili kuongeza uhalali wa utafiti. Ushuhudiaji umesaidia kufuatilia shughuli za ufundishaji darasani na umehusisha wanafunzi wote wa darasa zima. Aidha, ushuhudiaji ulifanyika zaidi ya mara moja kwa kila shule teule ili kupata data za kuaminika. Maktaba za shule teule zimechunguzwa ili kutathmini upatikanaji wa nyenzo za kusoma kama vile vitabu na namna wanafunzi wanavyotumia maktaba kwa kusoma.

Aidha, Nadharia ya Utamadunijamii ilitumika katika utafiti wetu. Nadharia hii iliasisiwa na Vygotsky, (1997). Pia nadharia hii inasisitiza umuhimu wa mwingiliano wa jamii katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Nadharia hii imetumika kwa sababu inadokeza umuhimu wa mwingiliano wa jamii na taasisi kama vile shule katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Hivyo, wanafunzi wanaweza kujifunza Kiswahili kama lugha ya pili nchini Rwanda kupitia mwingiliano wao na wanajamii katika matukio mbalimbali.

Nadharia hii ina mihimili miwili ambayo imeongoza makala yetu. Mhimili wa kwanza unahusu uunganishaji wa mawasiliano na shughuli za kijamii. Hii ina maana kwamba ili ujifunzaji lugha ufanyike kwa ufanisi, ni sharti kuhusishwa na hali halisi ya mawasiliano katika shughuli mbalimbali za kijamii. Shughuli hizo ni kama vile michezo, biashara, sherehe, dini na mengineyo. Mhimili huu ulisaidia kubainisha namna ufundishaji wa stadi za kusoma na kuandika unavyofanyika katika shule teule za sekondari katika wilaya ya Nyamagabe.

Mhimili wa pili unalenga kuhakikisha kuwa wanafunzi wanaunganisha nadharia na vitendo katika kujifunza lugha ili kufanikisha mawasiliano. Mhimili huu unadokeza kwamba ujifunzaji wa lugha ya pili unapaswa kufanyika katika mazingira rasmi ambapo kunakuwa na miongozo rasmi inayowekwa katika utendaji ili kuona ufaafu wake. Mhimili huu ulisaidia kuchunguza jinsi stadi za

kusoma na kuandika zinavyofundishwa na kueleza changamoto za utekelezaji wa ufundishaji wa stadi za kusoma na kuandika.

## 5.0 Hali ya Ufundishaji wa Stadi za Kusoma na Kuandika katika Somo la Kiswahili

Kusoma na kuandika ni stadi muhimu kwa sababu zinawasaidia wanafunzi katika mawasiliano, kuelewa maswali ya mtihani na kuyajibu ipasavyo (Khakasa, 2018). Hii inaashiria kwamba stadi hizi zinapaswa kufundishwa kwa ufanisi hususani katika masomo ya lugha ili kuwawezesha wanafunzi kupata matokeo mazuri darasani na Kiswahili kama nyenzo ya mawasiliano. Vilevile, **Silabasi ya Somo la Kiswahili** katika shule za sekondari nchini Rwanda inalenga kuwasaidia wanafunzi kukuza stadi za kusoma na kuandika. Haya ni malengo yaliyobainishwa:

i. Kusoma na kuhakiki kazi za fasihi simulizi hususan utanzu wa hadithi;
ii. Kusoma na kuelewa maandiko na vitabu mbalimbali vya Kiswahili vyenye taarifa ndefu ili kupata ujumbe uliomo;
iii. Kusoma na kuhakiki kazi za fasihi simulizi na fasihi andishi;
iv. Kusikiliza, kusoma na kuelewa kwa kina taarifa au habari mbalimbali kutokana na vyanzo vya habari zinazohusu masuala ya jamii kimasimulizi na kimaandishi;
v. Kuandika aina mbalimbali za insha za kimasimulizi (REB, 2020).

Malengo haya yanathibitisha kwamba stadi za kusoma na kuandika zinapaswa kutiliwa mkazo katika ufundishaji wa Kiswahili. Hii itawasaidia wanafunzi kukuza umilisi wa kimawasiliano ambao utaboresha matokeo yao ya darasani. Aidha, umilisi huu utawasaidia wanafunzi kushiriki kikamilifu na kufanikisha shughuli mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kisiasa zinazohitaji matumizi ya Kiswahili (REB, 2020).

### 5.1 Mbinu za Ufundishaji Stadi za Kusoma na Kuandika

Data za usaili na ushuhudiaji zinaonesha kwamba walimu wa Kiswahili wanatumia mbinu tofauti wanapofundisha stadi za kusoma na kuandika. Baadhi ya mbinu zilizotajwa ni usomaji wa kina, kuandika muhtasari wa kile wanachosikia na mbinu nyinginezo.

Mtoataarifa mmojawapo alieleza kwamba anapofundisha stadi za kusoma na kuandika, anawashirikisha wanafunzi katika usomaji wa kimya na mazoezi ya uandishi. Nukuu inayofuata inatoa maelezo zaidi.

> Ninafundisha stadi za kusoma na kuandika kupitia usomaji kimyakimya, kushirikisha wanafunzi katika mazoezi ya kuandika mmoja baada ya mwingine na kusoma kwa pamoja.

Nukuu hii inadhihirisha kwamba mtaotaarifa huyu anapofundisha stadi za kusoma na kuandika, anawasaidia wanafunzi kufanya kazi binafsi au kushirikiana baina yao. Hata hivyo, hakueleza hatua mahususi zinazoweza kufuatiliwa ili kufanikisha malengo ya ufundishaji. Hivyo, ni vigumu kuelewa ikiwa wanafunzi wanajifunza stadi za kusoma na kuandika kwa njia mwafaka.

Mtoataarifa mwingine anaeleza kwamba anatumia mbinu za ufundishaji wa stadi za kusoma na kuandika zinazolenga kutathmini zaidi kuliko kufundisha. Maelezo yake yanapatikana katika nukuu hii ifuatayo:

> Ninapofundisha stadi za kusoma na kuandika kwa wanafunzi wangu, huwa ninawasomea matini kisha, nikawaomba wanafunzi kuandika ninayoyasoma na kuwapa alama kulingana na wanayoyoaandika.

Mtoataarifa huyu anafundisha stadi za kusoma na kuandika kwa kuwasomea wanafunzi na kuandika kile anachosoma. Mbinu hii ni nzuri kwa sababu inatoa misingi kwa wanafunzi ya kusikiliza na kuandika, ila haiwasaidii wanafunzi kukuza stadi za kusoma. Aidha, mbinu hii haiwashirikishi wanafunzi katika mchakato wa ujifunzaji kwa sababu hawapati fursa kufanya kitendo cha kusoma. Kwa upande mwingine, kitendo kile cha kuandika kinatokana na matini inayosomwa na mwalimu. Mhimili wa pili wa Nadharia ya Utamadunijamii unaelekeza kwamba mwalimu anapofundisha stadi za kusoma na kuandika, anapaswa kuwasaidia wanafunzi kuunganisha nadharia na vitendo ili kufanikisha mawasiliano. Hivyo, wanafunzi wanapaswa kushirikishwa katika kazi za kusoma na kuandika ili kukuza stadi husika kwa ukamilifu.

Ili kupata data za nyongeza kuhusu suala hili, manaibu wakuu wa shule wanaohusika na masomo walihojiwa. Mahojiano yametoa taarifa kuhusu mbinu wanazotumia walimu katika ufundishaji wa stadi za kusoma na kuandika. Mmoja wao alieleza kwamba walimu wanatumia imla, uandishi wa muhtasari na kujibu maswali kwa mfumo wa insha kama mbinu za kufundisha stadi za kusoma na kuandika. Hii inaelezwa wazi katika nukuu ifuatayo:

> Katika shule hii wakati walimu wanapofundisha stadi za kusoma na kuandika, hutumia imla, uandishi wa muhtasari, kutoa majibu kwa kutumia mfumo wa insha kujibu, na usomaji binafsi wa mwanafunzi.

Nukuu ya mtoataarifa hapo juu inathibitisha mbinu za kufundisha stadi za kusoma na kuandika. Licha ya uzuri wake, mbinu hizi hazitoi fursa kwa wanafunzi kukuza uwezo wa kugundua namna bora ya kuandika na kusoma. John (2018) anaeleza kwamba mwalimu anapaswa kutumia mbinu zinazowashirikisha wanafunzi katika ugunduzi na tafakuri ili kukuza stadi za kusoma na kuandika.

Ufanikishaji wa kufundisha stadi za kusoma na kuandika unawahitaji walimu wa Kiswahili kutoa kazi kwa wanafunzi zinazochochea ubunifu, na hivyo kutumia maarifa ya darasani katika maisha halisi kuliko kufuata maelekezo kila wakati. Hoja hii inaungwa mkono na mhimili mmojawapo ya Nadharia ya Utamadunijamii usemao mwalimu anapaswa kuhakikisha kwamba wanafunzi wanaunganisha nadharia na vitendo katika kujifunza lugha ili kufanikisha mawasiliano.

Andalio la somo ni lazima lieleze wazi hatua za kufundisha stadi za kusoma na kuandika kwa kuzingatia somo lolote linalotarajiwa kufundishwa. Kwa mujibu wa Oser na Baeriswl (2001), walimu wanapaswa kukuza stadi za kusoma na kuandika kupitia somo wanaloandaa. Hii inatokana na kwamba, andalio la somo linaonesha mbinu za kufundisha ili kufanikisha malengo ya ujifunzaji yanayotarajiwa. Hata hivyo, data zilizokusanywa zimebainisha kwamba walimu wa Kiswahili hawafundishi stadi za kusoma na kuandika kikamilifu. Hii ni kwa sababu malengo ya ujifunzaji katika andalio la somo hayaoneshi wazi namna walimu wanavyopaswa kufundisha stadi hizi. Hii inathibitishwa na Kielelezo Na. 1 cha andalio la somo kifuatacho.

<table>
<tr><td>Muhula:</td><td>Tarehe:</td><td>Somo:</td><td>Kidato:</td><td>Mada:</td><td>Somo la:</td><td>Muda:</td><td>Idadi ya wanafunzi</td></tr>
<tr><td>wa kwanza</td><td>10/11/2021</td><td>Kiswahili</td><td>4 LLK</td><td>I</td><td>7 katika 45</td><td>Dakika: 80</td><td>45</td></tr>
<tr><td colspan="6">Aina ya wanafunzi wenye mahitaji ya kielimu watakaoshughulukiwa katika somo, idadi yao kulingana na mahitaji yao</td><td colspan="2">0</td></tr>
<tr><td colspan="2">Mada</td><td colspan="6">LUGHA YA KISWAHILI</td></tr>
<tr><td colspan="2">Uwezo uhitajiwao katika somo</td><td colspan="6">Kusikiliza , kuzungumza na kuandika kwa minajili ya kuelewa lugha na umuhimu wake kama chombo cha mawasiliano</td></tr>
<tr><td colspan="2">Somo lenyewe</td><td colspan="6">ALFABETI KATIKA KISWAHILI</td></tr>
<tr><td colspan="2">Malengo ya kujifunza</td><td colspan="6">Kwa kutumia vifungu mbalimbali, kufikia mwisho wa funzo, mwanafunzi aweze:<br>-Kuonesha kwa usahihi matumizi sahihi ya sauti za Kiswahili katika maandishi<br>-Kutumia msamiati wa Kiswahili kwa tahajia bora<br>-Kufurahia matumizi ya Kiswahili shuleni nan je ya shule</td></tr>
<tr><td colspan="4">Mahali mbapo somo litafundishiwa</td><td colspan="4">Somo litafundishiwa darasani</td></tr>
<tr><td colspan="4">Vifaa au zana kwa wanafunzi wote</td><td colspan="4">Kitabu cha mwalimu, kitabu cha mwanafunzi na kamusi</td></tr>
<tr><td colspan="2">Vitabu vya rejelea</td><td colspan="6">REB (2018). Kitabu cha Kiswahili IV. Kitabu cha Mwanafunzi & Mwalimu. Kigali.</td></tr>
<tr><td rowspan="3">Muda na hatua</td><td colspan="6">Mbinu za kufundisia na kujifunzia</td><td rowspan="3">Tafakuri tunduizi na maswala mtambuka vielezwe +maelezo mafupi</td></tr>
<tr><td colspan="6">Kwa kutumia vifungu vya habari tofauti, mwalimu atawawezesha wanafunzi kuhusisha mila na desturi mbalimbali katika kuaga na kumbulishana salamu, kuonesha kwa usahihi matumizi sahihi ya sauti za Kiswahili na kutumia msamiati husika kwa matamshi na tahajia bora kwa usahihi</td></tr>
<tr><td colspan="3">Wajibu wa mwalimu</td><td colspan="3">Wajibu wa mwanafunzi</td></tr>
<tr><td>Utangulizi<br>Dakika. 20</td><td colspan="3">Kuuliza maswali ya kukumbusha somo la awali</td><td colspan="3">Kujibu maswali maswali ya kukumbusha somo la awali</td><td rowspan="3">Mawasiliano katika lugha rasmi.<br>(Kupitia njia ya kujadiliana na kujibu maswali ya mwalimu katika makundi, wanafunzi watumie lugha rasmi ya Kiswahili)<br><br>Tafakuri tunduizi:<br>(wanafunzi kwa kutafuta maana ya matumizi ya kiambishi chenye dhana ya masharti)<br><br>Ujifunzaji wa muda mrefu</td></tr>
<tr><td>Somo lenyewe<br><br>Dakika: 50</td><td colspan="3">Kutoa tathmini tanguluzi<br><br>Kuwakaza wanafunzi kwenye makundi na kuwapatia wanavunzi tathmini endelezi<br><br>Kuchunguza ikiwa kazi wanafanywa na kutoa msaada kama unahitajika<br><br>Kuomba wanafunzi kwasilisha na kuwasaidia kusahihisha yaliyowasilishwa na kuyafanyia ufupisho</td><td colspan="3">Kujibu maswali ya tathmini tangulizi<br><br>Kukaa kwenye makundi na kujibu maswali ya tathmini endelezi<br><br>Kufanya kazi na kuomba msaada kwa mwalimu kama unahitajika<br><br>Kuwasilisha, kuungana mkono na mwalimu katika kusahihisha yaliyowasilishwa, kuyafanyia ufupisho na kuuandika madaftarini</td></tr>
<tr><td>Hitimisho<br>Dakika: 10.</td><td colspan="3">Kuoa tathmini jumuishi</td><td colspan="3">Kujibu maswali tathmini jumuishi</td></tr>
<tr><td colspan="2">Tathmini ya mwalimu</td><td colspan="6">Somo limefundishwa vizuri.</td></tr>
</table>

**Kielelezo 1:** *Mfano wa Andalio la Somo* (Data za Uwandani, 2022)

Kielelezo Na. 1 hapo juu kinaonesha kuwa andalio la somo la Kiswahili linahitaji kuboreshwa kwa kuondoa dosari zilizobainika. Dosari hizi zinajitokeza hasa kwenye vipengele vya *Uwezo Uhitajiwao katika Somo,* na *Malengo ya Kujifunza*.

Sehemu ya *Uwezo Uhitajiwao katika Somo* imeandikwa: "Kusikiliza, kuzungumza, kuandika kwa minajili ya kuelewa lugha na umuhimu wake kama chombo cha mawasiliano". Sehemu hii ina kasoro kutokana na kuwa haihusishi stadi za kusoma. Ili kuboresha sehemu hii, mwalimu angeandika: "kusikiliza, kuzungumza, kuandika na kusoma kwa madhumuni ya kuelewa lugha na umuhimu wake kama chombo cha mawasiliano".

Pia, *Malengo ya Kujifunza* hayajazingatia stadi ya kusoma. Malengo yangeandikwa kwa namna ya kuakisi vipengele vyote vya lugha. Hivyo, wangeandika: "Kwa kutumia vifungu mbalimbali, kufikia mwishoni mwa funzo, mwanafunzi ataweza:

i) Kuonesha kwa usahihi matumizi ya fonimu za Kiswahili katika matamshi na maandishi;
ii) Kutumia msamiati wa Kiswahili kwa matamshi na tahajia bora, na
iii) Kujivunia faida zitokanazo na kusoma na kuandika kwa ufasaha lugha ya Kiswahili.

Kutokana na data tulizokusanya, imebainika kwamba walimu wa Kiswahili hawafundishi stadi za kusoma na kuandika kwa ufanisi. Hali hii inaathiri vibaya umilisi wa mawasiliano miongoni mwa wanafunzi. Leticja (2015) anathibitisha kuwa ukosefu wa maandalizi mazuri ya masomo miongoni mwa walimu huathiri mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Hivyo, walimu wanapaswa kukuza uelewa wao wa kuandaa masomo ili waweze kufundisha stadi zote za lugha. Hii itawasaidia wanafunzi kuwa na umilisi wa mawasiliano ambao ni mojawapo ya malengo ya MEU.

Aidha, ufundishaji mwafaka wa stadi za kusoma na kuandika utafanikisha MEU. Mtaala huu unadhamiria kuwasaidia wanafunzi kuwa na umilisi wa mawasiliano unaohitajika katika miktadha mbalimbali ya maisha. Kwa mantiki hii, ilikuwa muhimu kuchunguza maoni ya walimu wa Kiswahili kuhusu MEU. Uelewa wao kuhusu dhana hii ni msingi wa utekelezaji wake. Walimu wenye maarifa kuhusu MEU wanaweza kufanikisha ufundishaji wa stadi za kusoma na kuandika, na hivyo kusaidia wanafunzi kuwa na umilisi wa lugha lengwa na stadi nyingine zinazohitajika katika maisha ya kila siku.

Maoni yaliyotolewa na walimu wa Kiswahili yameonesha kwamba baadhi yao hawaelewi vema maana ya MEU. Hii imedhihirishwa na maoni waliyoyatoa walipoulizwa kutoa fasili ya mtaala. Mmojawapo wa watoataarifa anafafanua

mtaala huu kama mambo yanayopangwa ili kufundishwa. Nukuu hii inatoa fasili ya mtaotaarifa huyo:

> Mtaala unaoegemea uwezo ni mambo yanayopangiliwa kwa ajili ya kufundishwa katika viwango mbalimbali vya elimu toka shule za msingi hadi vyuo vikuu. Mambo haya yanampa mtu ujuzi na maarifa yanayomwezesha kukabiliana na maisha kwa ujumla.

Nukuu hapo juu inadhihirisha kwamba mtoataarifa huyu ana uelewa kuhusu baadhi ya vipengele vya MEU. Pia, anashindwa kueleza kwa kina dhana ya mtaala. Hakuweza kufafanua kuwa unalenga kukuza ujuzi, maarifa, maadili na thamani ya wanafunzi ili kuwaandaa katika maisha halisi. Barman na Konwar (2011) wanatetea hoja hii kwa kueleza kwamba MEU unalenga kukuza stadi za maisha kama vile ubunifu, tafakuri tunduizi, mawasiliano, utafiti, ushirikiano pamoja na ujifunzaji endelevu miongoni mwa wanafunzi.

Kwa upande mwingine, mtoataarifa kutoka shule jirani alionekana kuwa na uelewa zaidi wa MEU. Kwake, mtaala huu unatoa nafasi kwa mwanafunzi kama mtekelezaji wa maarifa akisaidiwa na mwalimu kama mwelekezaji. Nukuu hii inaeleza:

> Mtaala unaoegemea uwezo ni mtaala unaompa mwanafunzi nafasi ya kukuza ujuzi na kipaji chake katika ujifunzaji. Mtaala huu unamfanya mwalimu kuwa mwelekezaji na manafunzi kuwa mtekelezaji wa maarifa ya darasani badala ya kuyaweka kichwani tu.

Kwa kurejelea nukuu hii, inaonekana kuwa mtaoataarifa huyu ana uelewa kuhusu MEU kama unamwezesha mwanafunzi kutumia maarifa anayojifunza darasani na kuyaweka vitendoni katika maisha halisi. Kazi ya mwalimu ni kumwongoza mwanafunzi katika mchakato huu. Hii inatetewa na REB (2015) ikisema kwamba, MEU una lengo la kumshirikisha zaidi mwanafunzi katika mchakato wa ujifunzaji ili aweze kutekeleza maarifa ya darasani katika maisha halisi.

Pia, uelewa tofauti wa walimu wa Kiswahili kuhusu MEU unaweza kuathiri utekelezaji wake darasani. Hii inatokana na kwamba walimu wenye uelewa mdogo wanaweza kushindwa kutekeleza mtaala vilivyo, huku wale wenye uelewa mkubwa wakitekeleza mtaala kikamilifu. Pamoja na uelewa wa walimu kuhusu MEU, walimu wanakabiliwa na changamoto tofauti wanapofundisha stadi za kusoma na kuandika. Sehemu inayofuata inazungumzia changamoto hizi.

### 5.2 Changamoto Zinazokabili Walimu Wanapofundisha Stadi za Kusoma na Kuandika

Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba walimu wa Kiswahili wanakutana na changamoto mbalimbali wanapofundisha stadi za kusoma na kuandika. Changamoto hizi zinatokana na wanafunzi na mazingira ya ufundishaji.

Changamoto ya kwanza ni ukosefu wa utamaduni wa kusoma na kuandika miongoni mwa wanafunzi. Mmojawapo wa watoataarifa anaeleza:

> Changamoto zinazotukabili tunapofundisha stadi za kusoma na kuandika ni ukosefu wa utamaduni wa kusoma na kuandika baina ya wanafunzi. Wanafunzi wanapopewa kazi za kuandika na kusoma wanashindwa kuzifanikisha. Baadhi ya wanafunzi wanaojaribu kufanya kazi hizi, wanakiuka kanuni za uandiahi sheria za kisarufi na uteuzi wa msamiati usio sahihi.

Nukuu ya mtoataarifa hapo juu inaonesha kwamba ukosefu wa mazoea ya kusoma na kuandika ni mojawapo ya changamoto kubwa zinazowakabili walimu wa Kiswahili. Wanafunzi wanashindwa kufanikisha kazi wanazopewa, jambo ambalo linaathiri ukuzaji wao wa stadi za kusoma na kuandika. Kadhalika, Gbadamosi (2007) anadokeza kwamba utamaduni wa kusoma huendelezwa kadiri mtu anavyosoma maandiko mbalimbali. Kukosekana kwa mazoea haya kunakwamisha ukuaji wa stadi hizi. Hivyo, ni dhahiri shahiri kwamba wanafunzi wanapaswa kupewa kazi za kusoma na kuandika ili kuchochea utamaduni huu miongoni mwa wanafunzi.

Changamoto ya pili ni ukosefu wa vifaa vya kufundishia stadi za kusoma na kuandika.Watoataarifa walieleza kwamba upungufu wa vifaa kama vile, vitabu ni changamoto kubwa. Mtoataarifa anaeleza:

> Changamoto inayonikumba ninapofundisha stadi za kusoma na kuandika ni ukosefu wa vitabu vya Kiswahili ninavyoweza kutumia wakati wa kufundisha. Unakuta mwalimu ana kitabu kimoja au viwili katika darasa la wanafunzi kati ya 20 na 30. Licha ya uchache wa vitabu hivi, hakuna kazi za kifasihi zinazoweza kupewa wanafunzi ili waweze kujisomea wenyewe.

Nukuu hii inaonesha wazi kwamba ukosefu wa vifaa unazuia walimu kufundisha kwa ufanisi stadi za kusoma na kuandika. Nkurunziza (2012) anaeleza kwamba wanafunzi wanaopata fursa ya kusoma vitabu vya hadithi nyumbani kwao ni asilimia tano tu huku asilimia sita wanapata vitabu maktabani au mahali pengine wanapoweza kuazima. Hii inaonesha kwamba kuna changamoto ya ukosefu wa vifaa vya kujifunzia lugha kwa walimu na wanafunzi.

Pia, data za ushuhudiaji uliofanyika zimebainisha changamoto hii. Ingawa kuna maktaba zenye vitabu mbalimbali, vitabu vya Kiswahili vilivyopo ni vile vinavyotumiwa na walimu katika ufundishaji. Hakuna vitabu vingine vya ziada kama vile hadithi fupi andishi au riwaya, ambavyo wanafunzi wanaweza kusoma kwa burudani au mazoezi ya kujifunza.

Changamoto huathiri wanafunzi moja kwa moja kumudu stadi hizi kwa kuwa hawapati fursa ya kujifunza kwa vitendo. Kama inavyodhihirishwa na mhimili mmojawapo wa Nadharia ya Utamadunijamii usemao kwamba ujifunzaji wa vitendo unapaswa kutiliwa mkazo katika ufundishaji wa lugha ya pili ili kukuza stadi za kusoma na kuandika.

Changamoto ya ukosefu wa vifaa vya kufundishia hususani vitabu, ilijitokeza pia katika wilaya nyingine nchini Rwanda. Kwa mfano, utafiti uliofanywa na Nyagatare, Tuyishimire na Mlaga (2023) ulibainisha kwamba walimu wa Kiswahili wanakutana na changamoto ya upungufu wa vitabu vya fasihi vya kutumia katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili.

Mashaza (2017) anasisitiza kuwa uwepo wa vifaa vya kufundishia ni mojawapo ya sharti la muhimu la kufanikisha MEU. Upungufu wa vifaa hivi, unakwamisha ufundishaji wa Kiswahili hasa stadi za kusoma na kuandika. Hivyo, ni muhimu kuhakikisha kwamba vitabu vya Kiswahili vinapatikana ili kufanikisha ufundishaji wa stadi hizi.

Changamoto ya tatu ni ukosefu wa motisha kwa wanafunzi ya kusoma na kuandika. Hali ya ukosefu wa motisha imedhihirishwa na mmojawapo wa watoataarifa kama ifuatavyo:

> Changamoto nyingine inayotukumba wakati wa kufundisha stadi za kusoma na kuandika ni ukosefu wa motisha miongoni mwa wanafunzi. Wanafunzi wangu wanapenda Kiingereza zaidi kuliko Kiswahili. Hii inatokana na kwamba wengi walijifunza lugha ya Kiingereza kuanzia shule za chekechea wakati Kiswahili wameanzia shule za sekondari tu. Kwa hiyo, uwezo wao wa kuandika na kusoma upo kwa kiwango cha chini.

Nukuu ya mtoataarifa huyu inaonesha kwamba wanafunzi wanakosa motisha ya kujifunza stadi za kusoma na kuandika kutokana na usuli wao wa kujifunza Kiswahili. Hali hii imethibitishwa na mmojawapo wa manaibu wakuu wa shule wanaohusika na masomo akisema:

> Miongoni mwa changamoto zinazowakumba walimu wanapofundisha Kiswahili ni ukosefu wa motisha miongoni mwa wanafunzi. Wanafunzi wetu wana shida ya kukosa msamiati katika lugha ya Kiswahili. Hii inatokana na kwamba wanafunzi hawa wanaanza kujifunza lugha hii wanapofika shule za sekondari (kidato cha kwanza). Zaidi ya hayo, kwa kiwango hiki, Kiswahili hakitathminiwi katika mitihani ya taifa ya kidato cha tatu kama masomo mengine. Kwa hiyo, wanafunzi na hata walimu hawaweki mkazo kwenye lugha hii kama wanavyofundisha Kiingereza.

Nukuu hii inaonesha kwamba wanafunzi wanakosa motisha ya kujifunza Kiswahili ili kukuza stadi za kusoma na kuandika kutokana na hali ya lugha hii nchini Rwanda. Kwa mfano, kutotahiniwa kwa Kiswahili katika mitihani ya kitaifa ya wanafunzi wanaomaliza kidato cha tatu kunasababisha wanafunzi kutokiwekea mkazo Kiswahili. Walimu pia wanapuuza ufundishaji wake katika kiwango hiki. Hii inathibitishwa na mtoataarifa mmojawapo anaposema:

> Mara nyingi wanafunzi wanapofika katika mwaka wa tatu, wanatilia mkazo zaidi masomo ambayo watafanya katika mitihani ya kitaifa. Masomo yasiotahiniwa katika mtihani wa kitaifa ikiwemo Kiswahili, wanayaona kama anawapotezea muda tu. Hivyo, mara nyingi tunaamua kugawa vipindi vya Kiswahili kwa walimu wengine.

Nukuu hii inathibitisha ulazima wa kuhakikisha Kiswahili kinawekewa mkazo wa kitaaluma ikiwa ni pamoja na kuanza kutahiniwa katika mitihani ya kitaifa ya kidato cha tatu ili kukuza umilisi wa stadi za kusoma na kuandika.

Data zilikokusanywa zimebainisha kwamba walimu wanakutana na changamoto tofauti kama vile ukosefu wa vifaa vya kufundishia na motisha. Hivyo, makala yetu yametoa mapendekezo yanayoweza kutumiwa na walimu ili kukabiliana na changamoto hizi kwa ufanisi.

## 6.0 Mapendekezo ya Kufundisha Stadi ya Kusoma na Kuandika

Kulingana na changamoto zilizobainishwa, mapendekezo yafuatayo yanaweza kusaidia katika ufanisi wa stadi za kusoma na kuandika.

### 6.1 Utumiaji wa Modeli ya Andaa-Shiriki -Tafakari

Walimu wa Kiswahili wanaweza kutumia modeli hii wanapofundisha stadi za kusoma na kuandika ili kuwasaidia wanafunzi kushirikiana na kuelewa somo linalofundishwa kwa kina. Modeli ya andaa-shiriki-tafakari inaweza kutumika pale mwalimu anapotoa maswali kwa wanafunzi kabla na wakati wa somo. Miongoni mwa maswali ambayo yanaweza kutolewa kwa wanafunzi ni:

i. Unafikiri utajifunza nini kwenye somo la leo?
ii. Unaelewa nini kuhusu somo ambalo tutajifunza leo?
iii. Una swali gani kuhusu somo tunalotarajia kujifunza?
iv. Ni uwezo gani unakusudia kuupata baada ya kujifunza somo la leo?

Baada ya kujibu maswali haya, wanafunzi huwekwa katika makundi ya watu hadi watano ili washirikishane katika majibu. Kila mwanafunzi anapaswa kusoma majibu yake katika kundi. Hii inawasaidia wanakikundi kuelewa mtazamo wa kila mwanafunzi na kujadili kwa kina. Baada ya kufanya mjadala, wanakikundi wanatakiwa kusanisi majibu yao na kuyaandika katika karatasi moja ya kundi. Kisha kundi hilo hushirikisha majibu yao kwa darasa zima.

Wakati wa kuunda makundi, mwalimu anapaswa kuhakikisha kwamba kila mwanakikundi anachangia katika kukamilisha kazi husika kuliko mwanafunzi mmoja kufanya kazi kwa niaba ya kundi. Hii inajenga ushirikiano, mawasiliano na uwajibikaji miongoni mwa wanafunzi (Tuyishimire na Mlaga, 2022).

Vilevile, wanafunzi wanaweza kupewa mazoezi ya ufahamu na utungaji wa kazi za kubuni kama vile insha kuhusu mada zinazohusiana na shughuli za kila siku kama vile siasa, kilimo na ufugaji, uchumi, biashara, dini na kazi za kifasihi. Baada ya utungaji wa kazi hizi, wanafunzi wanaweza kushirikishwa kuhakiki kazi zilizoandikwa na wenzao. Hapa wanafunzi wanaweza kutakiwa kuandaa ripoti ya uhakiki ambao wamefanya kwa kuonesha mawazo makuu yaliyopo katika kazi husika, maswali yanayoweza kuulizwa katika kazi, funzo lililomo, na namna ya kuboresha zaidi kazi husika. Aidha, wanafunzi wanaweza kushirikishwa kuwasilisha kazi ambazo wametunga.

Mwalimu akifuata utaratibu huu, ataweza kufanikisha malengo yake ya kufundisha stadi za kusoma na kuandika. Sharon (2018) anaunga mkono modeli hii akisema kwamba modeli ya andaa-shiriki-tafakari inawasaidia wanafunzi kukuza stadi za kusoma na kuandika na kuwawezesha wanafunzi kujifunza kwa vitendo na hivyo kuwa na umilisi wa mawasiliano. Suala hili linashadidiwa pia na mhimili mmojawapo wa Nadharia ya Utamadunijamii ambao unasisitiza ujifunzaji unaoweka mkazo kwenye vitendo ili kuwasaidia wanafunzi kuhusisha darasa na maisha halisi.

### 6.2 Utumizi wa Usomaji na Uandishi Changizi

Walimu wa Kiswahili wanaweza pia kutumia usomaji na uandishi changizi wanapofundisha stadi za kusoma na kuandika. Mwalimu anatoa mfano wa matamshi na tahajia bora kwa wanafunzi kisha wanafunzi wanaiga mfano alioutoa. Ili kutekeleza mbinu hii, mwalimu hana budi kufuata hatua tatu zifuatazo:

Mosi, mwalimu achague maandishi ambayo yanaweza kuwa riwaya, shairi au maandishi mengine yanayohusu mada ambayo atafundisha. Mwalimu awatangulie kusoma kwa sauti na wao wafuate. Baada ya kuridhika na usomaji wa wanafunzi kama kundi, mwalimu ateue wanafunzi kusoma kila mmoja aya moja tofauti ili kujiridhisha na uwezo wao wa kusoma. Ahakikishe wanafunzi wote darasani wanaweza kusoma kwa ufasaha kifungu husika.

Pili, mwalimu awashirikishe wanafunzi kusoma kazi ileile kwa kupewa muda wa kutosha. Kazi hii inaweza kufanyika katika makundi au kufanywa na mwanafunzi mmojammoja. Kupitia usomaji wa kazi hizi, wanafunzi watapata fursa ya kugundua hali za binadamu na masuala mbalimbali ya kijamii yanayojitokeza katika kazi husika. Vilevile, usomaji wa kazi utawasaidia wanafunzi kujifunza lugha, kukuza fikra zao na kuyatumia yale wanayojifunza katika maisha halisi.

Baada ya usomaji, wanafunzi wanapaswa kubainisha msamiati mpya na mwalimu awaongoze kuutolea ufafanuzi. Aidha, wajifunzaji washirikishwe kubainisha lengo la andiko, kudokeza mawazo makuu yaliyopo katika andiko na kudhihirisha muundo na mtindo wa andiko.

Tatu, mwalimu awashirikishe wanafunzi kuigiza au kuwasilisha kazi ambazo wamesoma ili kuelewa zaidi ujumbe wa kazi husika. Uigizaji huu unawasaidia wanafunzi kuhusisha maarifa ya darasani na maisha halisi. Hii inathibitishwa na mhimili wa kwanza wa Nadharia ya Utamadunijamii usemao kwamba mwalimu anapaswa kuunganisha ufundishaji lugha na mazingira halisi ya kijamii.

Kazi za aina hii zinaweza kuwasaidia wanafunzi kwa namna mbili. Mosi, kukuza stadi za lugha zikiwamo kusoma na kuandika ambazo, ni muhimu katika mawasiliano. Pili, kuwasaidia wanafunzi kupata kichocheo cha kutunga kazi zao wenyewe. Kazi zinazotungwa na wanafunzi hawa zinaweza kuhaririwa na kutumiwa katika ufundishaji. Wanafunzi wanaposhiriki katika kazi hizi, wanakuza vipaji vya uandishi. Hatimaye, wanaweza kuvitumia kuwa waandishi mashuhuri na kupata pesa kupitia maandishi yao.

## 7.0 Hitimisho

Kupitia makala haya, imebainika kwamba walimu wa Kiswahili hawafundishi stadi za kusoma na kuandika kikamilifu ili kutekeleza MEU. Changamoto hii inatokana na kwamba walimu wanatumia mbinu za ufundishaji ambazo haziwashirikishi ipasavyo wanafunzi kukuza stadi. Vilevile, walimu wanakutana na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na ukosefu wa vifaa vya kufundishia na wanafunzi kutokuwa na utamaduni wa kusoma.

Hivyo basi, makala yametoa mapendekezo ya matumizi ya modeli ya andaa-shiriki-tafakari na kazi za usomaji na uandishi changizi katika ufundishaji wa stadi hizi ili kufanikisha ufundishaji wa stadi za kusoma na kuandika. Mapendekezo haya yatawasaidia wanafunzi pia kuwa na uwezo wa tafakuri tunduizi, ubunifu, utafiti, ushirikiano ambao ni muhimu katika kufanikisha malengo ya MEU.

## Marejeleo


Alderson, C. (2000) *Assessing Reading*. Cambridge: Cambridge University Press.

Barman, A. na Konwar, J. (2011) "Competency Based Curriculum in Higher Education: A necessity Grounded by Globalisation". *Romanian Journal for Multidimensional Education.* Juz. Na. 3(6): 7-17. Inapatikana katika https://shorturl.at/Re15A. Ilisomwa tarehe 15 Machi 2021.

Bojovic, M. (2008) "Development of Reading Skills in Second Language Learning and Teaching". *International Journal of Psychology*, Juz. Na. 43(4): 223-223.

Creswell, J.W. (2012) *Educational Research: Planning, Conducting, and Evaluating Quantitative and Qualitative Research* (Toleo la 4). New York: Pearson.

Dalaney, Y.A. (2008) "Investigating the Reading-to-Write Construct. Education. *Journal of English for Academic Purposes,* Juz. Na. 7(3): 140-150. Inapatikana katika https://shorturl.at/rRzLG. Ilisomwa tarehe 15 Aprili 2021.

Fema, B.M. (2003) "Problem of Teaching English Language in NCE Programme. *Azare Journal of Education*. Juz. Na. 4(1):107-112.

Gardner, R.C. (2000) "Correlation, Causation, Motivation and Second Language Acquisition", *Canadian Psychology,* Juz. Na. 41(1):10-24. Inapatikana katika https://shorturl.at/Dj6zx Ilisomwa tarehe 15 Aprili 2021.

Gbadamosi, T. (2007) "Library Reading Culture and Students Academic Performance in Secondary School in Oyo State". *Middle Belt Journal of Library and Information Science*, Juz. Na. 7(2): 42-58.

Harmer, J. (2004) *How to Teach Writing*. England: Longman.

John, P. (2018) "Constructivism: Its Implications for Language Teaching and Second-Language Acquisition". *Education and Development*. Inapatikana katika https://shorturl.at/WoauP. Ilisomwa tarehe 12 Januari 2022.

Jonson, R. (2001) "Teacher Learning in Second Language Teacher Education: A Socially-Situated Perspective". *Rev. Brasileira de LingUistica Aplicada*, Juz. Na. 1(1): 53-69. Inapatikana katika https://shorturl.at/lsL4d. Ilisomwa tarehe 08 Juni 2022.

Khakasa, L.S. (2018) *Mikakati ya Kufundisha Stadi ya Kusoma kwa Kutumia Vitabu vya Hadithi katika Shule za Msingi za Kaunti ya Kakamega Nchini Kenya*. Tasnifu ya Uzamili_(Haijachapishwa). Nairobi: Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro. Inapatikana katika https://feji.us/y3x6y6.

Kipacha. A. (2003) *Lahaja za Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Kitchakarn, O. (2014) "Developing Writing Abilities of EFL Students Through Blogging". *Turkish Online Journal of Distance Education*. Juz.Na.15(4):34-47. Inapatikana katika https://shorturl.at/bm07E. Ilisomwa tarehe 08 Julai 2021.

Leticja, P.G. (2015) "Factors that Affect Effective Planning Skills of the Teacher in the Classrooms". *Academic Journal of Interdisciplinary Studies*. Juz. Na. 4(3): 560-564. Doi:10.5901/ajis.2015.v4n3s1p560. Inapatikana katika https://shorturl.at/I60HL. Ilisomwa tarehe 08 Aprili 2021.

Mashaza, L.G. (2017) "Theoretical Perspectives on Critical Thinking Teaching: Reflections from Field Experiences from a Norwegian Lower Secondary School in Comparison to Tanzanian Secondary School Teaching Practices". *Journal of Education and Learning*, Juz. Na. 11(3): 312-318.

Inapatikana katika https://shorturl.at/lvRoG. Ilisomwa tarehe 08 Aprili 2021.

Miricho, E. (2008) *Distinction Kiswahili*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Moradi, M. (2019) "Teacher's Attitudes Towards the Effects of Lesson Plan on Classroom Management: A Case Study of Sufi Sahab Zakur High School". *American International Journal of Social Science Research,* Juz.Na. 4(2): 112-120. Inapatikana katika https://shorturl.at/QDw8d. Ilisomwa tarehe 08 Mei 2021.

Mulenga, I.M. na Kabombwe, Y.M. (2019) "Understanding a Competency-Based Curriculum and Education: The Zambian Perspective". *Journal of Lexicography and Terminology,* Juz. Na. 3(1):106-134. Inapatikana katika https://shorturl.at/KRuae. Ilisomwa tarehe 05 Aprili 2021.

Nkurunziza, F.C. (2012) *Reading Culture in Rwandan Community: Benefits and Challenges*. Inapatikana katika file:///C:/Users/user/Downloads/Reading_Culture_in_Rwandan_community_Ben.pdf. Ilisomwa tarehe 10 Julai 2021.

Nzima, I. (2016) *Competence-Based Curriculum (CBC) in Tanzania: Tutors' Understanding and their Instructional Practices*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Linnaeus, Växjö. Inapatikana katika https://rb.gy/wglm1o.

Oser, F. na Baeriswyl, F. (2001) "Choreographies of Teachings. Bridging Instruction to Learning". Katika Richardson, V. (Wah.), *Choreographies of Teachings. Bridging InstruCtion to Learning* (Toleo la 4). Washington: American Educational Research Association. kur. 1031-1085.

REB. (2015) *Competence Based Curriculum: Curriculum Framework Pre-primary to Upper Secondary*. Kigali: REB.

REB. (2022) *Muhtasari wa Somo la Kiswahili Mchepuo wa Lugha* (LFK). Kigali: REB

Ruterana. P, C (2012) "Enhancing the Culture of Reading in Rwanda: Reflections by Students in Tertiary Institutions", *The Journal of Pan African Studies*, Juz.Na.5 (1): 35-54.

Sharon, L. (2018) *Strategies for Teaching Reading na Writing Across Content Areas*. Inapatikana katika https://feji.us/b2sz2d. Ilisomwa tarehe 12 Machi 2021.

Tremblay, M.A., Blanchard, C.M., Taylor, S., Pelletier, L.G. na Villeneuve, M. (2009) "Work Extrinsic and Intrinsic Motivation Scale: Its Value for Organizational Psychology Research", *Canadian Journal of Behavioural Science*, Juz. Na. 41(4): 213-226. Inapatikana katika https://shorturl.at/Vf0uT. Ilisomwa tarehe 10 Septemba 2021.

Tuyishimire, L. na Mlaga, W. (2022) "Matumizi wa Fasihi katika Ukuzaji wa Tafakuri Tunduizi". *Jarida la CHALUFAKITA*, Juz. Na. 3(1): 93-120. Inapatikana katika https://shorturl.at/3IblK. Ilisomwa tarehe 26 Desemba 2021.

Tuyishimire, L. na Mlaga, W.K. (2023) "Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la Kiswahili Unaozingatia Stadi ya Tafakuri Tunduizi: Mifano kutoka Shule Teule za Sekondari Wilayani Nyagatare". *Jarida la Mulika*, Juz. Na. 42(2). 164-183. https://doi.org/10.56279/mulika.na42t2.2

Vygotsky, L. (1978) *Mind Society*: *The Development of Higher Psychological Process*. Cole, M. Steiner, V. Scriber, S. na Souberman, E. (Wah.), E. Cambridge, Massachuttes na London: Havard University Press.

William, G. na Fredricka, L.S. (2013) *Teaching and Researching Reading: Applied Linguistics in Action Series.* New York: Routledge.

Zaiter, A.W. (2019) "Reading and Writing Skills: The Challenges of Teaching at College Level". *Addaiyan Journal of Arts, Humanities and Social Sciences*, Juz. Na. 1(10): 41-51. Inapatikana katika https://shorturl.at/H5j6u. Ilisomwa tarehe 08. Desemba.2021.